
# TUTATUE MATATIZO YETU WENYEWE



Kimetolewa na:

IDARA YA ELIMU KWA UMMA,
TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA,
S.L.P. 20679. DAR ES SALAAM

# TUTATUE MATATIZO YETU WENYEWE

# TUTATUE MATATIZO YETU WENYEWE

IDARA YA ELIMU KWA UMMA
TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA
S.L.P. 20679, DAR ES SALAAM

© 1983 Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

Picha zimechorwa na:
Patric George wa
ALPHA ARTS,
DAR ES SALAAM.

Kimepigwa chapa na:
Idara ya Elimu kwa Njia ya Posta,
S.L.P. 9213,
Dar es Salaam.

# Y A L I Y O M O

1. UTANGULIZI ... ... ... ... ... ... vi

2. MAZUNGUMZO KATIKA FAMILIA YA MZEE OLE LENGAI 1

3. WANAKIJIJI WAJADILI MATATIZO .. ... ... 8

4. WANAKIJIJI WAALIKA WATAALAMU .. ... ... 13

5. UFUMBUZI WA MATATIZO ... ... ... ... 18

6. MAJINA YA WASHIRIKI ... ... ... ... 26

# UTANGULIZI

Huu ni mfululizo maalum wa vitabu ambavyo vimeandikwa kwa ajili ya watu wazima waliofika kiwango cha Elimu ya Msingi.

Vitabu hivi huandikwa chini ya ushirikiano baina ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na Chama cha Elimu ya Watu Wazima cha huko Ujerumani (DVV).

Madhumuni halisi ya mpango huu ni kuwawezesha watu wazima kupanua mawazo katika fani mbalimbali zenye mwelekeo wa maendeleo kisiasa, kiuchumi pamoja na kiutamaduni. Lengo ni kumfanya huyo mtu mzima atambue matatizo na kutafuta njia mbalimbali za kuyakabili matatizo hayo.

Vitabu hivi vimeandikwa kwa lugha rahisi na kwa mitindo mbalimbali. Tunategemea kuwa wasomaji watafaidika na yaliyomo.

E.N. Ntirukigwa
Kaimu Mkurugenzi
TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA

## SURA YA KWANZA

## MAZUNGUMZO KATIKA FAMILIA YA MZEE OLE LENGAI

Mzee Ole Lengai ni mtu mwenye nguvu nyingi. Ana umri wa miaka hamsini. Anakumbukwa sana kutokana na sifa zake za uanzilishi wa kijiji cha Kisongo. Kijiji hicho kipo magharibi mwa mji wa Arusha, kando ya barabara kuu iendayo Dodoma. Ole Lengai ana mke na watoto watatu. Mtoto wake wa kwanza anaitwa Naisoi ambaye ni wa kike, mtoto wake wa pili ni wa kiume anaitwa Loitore, na wa mwisho ni wa kike anaitwa Mangare.

Wakazi wa kijiji cha Kisongo hujishughulisha na kilimo, ufugaji na wachache wao hujishughulisha na biashara ndogo ndogo mjini Arusha. Maendeleo ya kijiji hicho hayajasonga mbele sana, hii imesababishwa na ukame wa kijiji hicho.

Kwa kawaida Mzee Ole Lengai anaamka alfajiri na mapema kwenda shambani. Mzee huyu analima mahindi, maharage na ufuta kidogo pembeni mwa shamba lake. Mke wake humfuata shambani baada ya kumtayarisha mtoto wake wa mwisho kwenda shuleni.

Jua likianza kuwa kali Mama Naisoi huanza kukusanya mabua makavu ya mahindi na magugu kwa ajili ya kupikia chakula cha mchana na jioni. Mara nyingi hufanya hivyo akikosa kuni na mkaa.

Jumamosi moja palipambazuka vizuri na ndege walikuwa wakiimba kwa sauti nzuri za kufurahisha. Mama Naisoi na mumewe walielekea shambani kabla hapajapambazuka vizuri. Kwa mbali majembe yalisikika yakitifua barabara. Jasho jembamba lilikuwa likiwatiririka Mzee Lengai na mkewe. Mzee Lengai alielekea nyumbani kwa jirani yake Mzee Mboyo ambaye alikuwa balozi kwa mazungumzo mafupi ya faragha.

Kwa kuwa siku ya Jumamosi hawarudi shambani mchana, alirudi nyumbani saa 9 jioni. Alipofika alikuta chakula

bado hakijawa tayari, kwa ghadhabu kuu alimwuliza mkewe, "Ninalima mara moja kwa mwaka, tena zao la chakula tu, iweje hadi saa hii hujaivisha chakula?"

Mkewe alimjibu kwa upole na wingi wa upendo, "Mume wangu mpendwa, moto unaotumika ni hafifu sana; isitoshe kupata kuni siku hizi ni sawa na kuokota dhahabu."

Mzee Lengai alijiinamia na kuendelea kuwaza.

Saa kumi ilipowadia chakula kilikuwa tayari. Wote walikaa na kuanza kula kwa furaha baada ya njaa kuwasokota kwa muda mrefu. Muda mfupi baada ya chakula Balozi Mboyo alibisha hodi na kukaribishwa na mzee mwenzie. Mgeni wake alimfikia na kumshauri juu ya kuendelea na kisomo chenye manufaa. Mzee Mboyo alikuwa ameshtushwa na mahudhurio mabaya ya wanakisomo wa shina lake.

Baadaye waliendelea kuzungumzia tatizo la mavuno haba, ambayo mara nyingi wanavuna baada ya kilimo cha masika tu.



Ilikuwa ni desturi ya wazee hawa na jirani zao ku-

cheza ngoma wakati wote wa misimu ya baridi na kiangazi. Waliamini kuwa misimu hiyo haifai kabisa kwa kilimo cha mazao ya chakula na biashara. Walianza kupanga taratibu ya ngoma zitakazochezwa kwani msimu ulikuwa unakaribia. Punde si punde Mama Naisoi alikatiza mazungumzo yao. Alimtaka balozi amfahamishe utaratibu wa kazi za Jumatatu katika shamba lao la Ushirika. Mzee Lengai alidakia mazungumzo hayo bila kuchelewa na kumweleza balozi kuwa yeye na mke wake watafika shambani mnamo saa tatu asubuhi. Balozi alipomwuliza kwa nini wafanye hivyo. Alimjibu na kumwambia, "Wanakijiji wengi hutega kazi za mseto na kuzifanya kiholela. Hata wataalam vijijini na mijini utendaji wao wa kazi hautoshelezi." Mazungumzo yaliendelea kwa muda mrefu. Machweo yalipowasili waliagana.

Mzee Mboyo alipitia kwa jirani yake mwingine kumshawishi ajiunge tena na kisomo baada ya kufaulu hatua ya nne. Balozi hakupendezwa na uamuzi wa wanakijiji waliofaulu hatua ya tatu na ya nne kuacha kisomo.

Alipofika alimkuta jirani yake anasikiliza redio, kipindi cha MKULIMA WA KISASA. Baada ya kuamkiana, walielezana matatizo ya kijiji chao, kwa ghafla mazungumzo yao yalikatishwa katikati. "Fedha za kigeni zinatuletea dawa za mifugo yetu na za watu, mashine za aina mbalimbali na mafuta ya mashine kutokana na mazao ya biashara." Redio ilisema. Wazee hawa hawakuamini bali waliamua kusubiri kuwauliza wataalam wao katika mkutano wa kijiji.

Hatimaye wazee hawa wawili hawakuelewana juu ya kuendelea na kisomo cha kujiendeleza. Balozi aliambiwa kwamba siku za kisomo katika wiki ndizo yeye huzitumia kwenda msituni ambako ni kilometa thelathini. Huko huwa anakata nguzo za kujenga boma la pili na kukata magogo ya kuchoma mkaa. Balozi na mwenyeji wake hawakuagana kimila kama ilivyo desturi yao. Aliondoka kwa masikitiko makubwa huku akiumwa njaa kwani hakukaribishwa chakula katika nyumba yoyote.

Ilikuwa siku ya Jumanne alfajiri na mapema mzee

Lengai na mkewe waliamka baada ya uchovu wa kazi za jana walizozifanya katika shamba la ushirika. Mzee Lengai alikwenda shambani kwake. Mama Naisoi alikwenda kutafuta kuni siku hiyo. Kuni zinapatikana kwa shida sana katika kijiji chao. Kwa hiyo yeye aliamua asiende shambani siku hiyo. Mnamo saa sita mchana Mama Naisoi alirudi nyumbani na mzigo wa kuni. Alichelewa kurudi kwa sababu kuni zenyewe wanazipata mbali sana. Mama Naisoi aliendelea na shughuli zake za upishi. Aliwasha moto na kutenga nyama jikoni. Alipomaliza kukaanga nyama alisonga ugali. Hakuweza kusubiri mpaka mumewe na wanawe warudi nyumbani kutokana na shida ya kuni.

Jioni baada ya jua kuzama Mzee Lengai alirudi nyumbani kutoka shamba. Kwa sababu alikuwa amechoka, alimwambia mkewe amtayarishie maji ya kuoga. Alipomaliza kuoga alitafuta shati safi avae. Lakini hakupata kwani yote yalikuwa machafu. Alimwita mkewe na kumwuliza kwa nini hajafua nguo zake. Mkewe alimjibu na kumwambia kuwa sabuni imekwisha. Ilimbidi avae shati chafu lililokuwa linanuka jasho.

Mzee Lengai alikaa ukumbini. Mkewe akaleta chakula na kumkaribisha mezani. Mama Naisoi na wanawe wawili, Naiso na Mangare walikula jikoni. Mzee Ole Lengai alizoea kula pamoja na mwanae wa kiume aitwaye Loitore, lakini hivi sasa yuko mjini. Baada ya muda si mrefu hodi ilisikika kutoka nje. Mzee Lengai aliitika, "Karibu." Mzee Mboyo akaingia. Walisalimiana vizuri.

Mzee Lengai alimwita mkewe na kumwambia awapikie chai. Mama Naisoi alimjibu mumewe na kumwambia sukari ilikwisha asubuhi.

"Kwa kweli siku hizi kuna tatizo sana la upatikanaji wa sukari," Mzee Mboyo alisema.

"Kwa kweli siku hizi kuna tatizo la vitu muhimu kwa ujumla. Nilipomaliza kuoga jioni nimetafuta shati safi la kuvaa nikakosa kwani yote ni machafu. Naagiza mke apike chai, sukari hamna! Kila siku tunakula ugali, mihogo na viazi tu; mchele hamna. Nikisema nifungue redio nisikilize hata taarifa ya habari, betri zimeisha, redio inanguruma tu. Kwa kweli mambo ni magumu," Mzee Ole

Lengai alinung'unika.

"Duka la ushirika tunalo na sijui kwa nini mambo yanakuwa hivyo?" Mzee Lengai aliuliza.

"Mimi naona ugawaji una upendeleo. Japo vitu vinavyokuja siyo vingi na pia haviji mara nyingi, lakini wangevigawa kwa mpangilio mzuri mambo yangekuwa yanaridhisha kiasi", Mzee Mboyo alijibu.

"Ah, nimekumbuka hivi karibuni kuna mkutano wa kijiji, kwa hiyo tutaweza kuuliza maswali haya," Mzee Lengai alisema.

"Maongezi yamekuwa matamu mpaka nimesahau kukueleza kuwa mke wangu amejifungua mtoto wa kiume," Mzee Mboyo alisema.

"Nakupa hongera, lakini nakumbuka kwamba mkeo aliejifungua mtoto mwaka juzi, mwaka jana na hata mwaka huu tena amejifungua?" Mzee Lengai aliuliza kwa mshangao.

"Ni kweli usemavyo," alijibu Mzee Mboyo. Mzee Lengai alishangaa kwa kujulishwa kujifungua kwa mke wa Mzee Mboyo. Kila mwaka mkewe Mboyo anazaa na hivyo inamzuia hata asiweze kushiriki katika shughuli za maendeleo. Na sasa hivi wana watoto sita. Wote wamepishana umri wa mwaka mmoja mmoja. Mzee Mboyo hawezi kumudu kilimo cha peke yake wakati familia yote inamtegemea yeye. Na mkewe hawezi kusaidia kutokana na kutokufuata uzazi wa majira. Kwa hiyyo maisha ya Mzee Mboyo yanakuwa ni ya matatizo sana.

Baada ya kila mmoja kuwa kimya kwa muda mfupi Mzee Mboyo alimwambia Mzee Lengai kuwa anamwomba mtoto wake wa kiume aitwae Loitore aende akamletee mkewe kuni kesho yake. Watoto wa Mboyo ni wadogo hawawezi kwenda mbali kutafuta kuni. Lengai alimwambia kuwa Loitore tangu amalize darasa la saba aliaga anakwenda Arusha mjini kwa mjomba wake. Alimwandikia barua arudi lakini hakurudi. Aliwaandikia na kuwaeleza kuwa anatafuta kazi mjini.

"Kwa kweli huu ni mtindo wa vijana wengi hapa kijijini. Hata mtoto wa Mzee Kisivani, huu ni mwaka wa pili hajaja nyumbani, wala wazazi wake hawajui anafanya kazi gani huko mjini, maana hata barua hatumi kwa wazazi



wake. Lakini sikuwa na habari kuwa Loitore nae ameki mbilia mjini," Mzee Mboyo alisema.

"Ni vijana wengi wa kijiji hiki wakishamaliza shule za msingi tu wanakimbilia mjini. Vijana wengi ninaowafahamu ambao walimaliza darasa la saba mwaka jana hapa kijijini wamekimbilia mjini," Mzee Lengai alisisitiza.


Baada ya mazungumzo marefu wazee hawa waliamua kuwa watajaribu kuchunguza kwa wanakijiji wenzao kama nao wana matatizo kama yao. Mama Naisoi nae alisema atajaribu kuwauliza wanawake wanzie hapo kijijini kama wanakabiliwa na matatizo kama yao. Pia atawashawishi kuja

kuyaeleza na kuyajadili katika mkutano wa kijiji utakao-fanyika hiyi karibuni. Mzee Mboyo aliaga na kwenda zake nyumbani.

Baada ya uchunguzi wao waliona matatizo hayo yanawa-kabili wanakijiji wengi siyo wao tu. Kwa hiyo walingoja kwa hamu sana siku ya mkutano iwadie.

## SURA YA PILI

## WANAKIJIJI WAJADILI MATATIZO



Siku iliyofuata ilikuwa ndiyo siku ya Mkutano. Wanakijiji wote wa kijiji cha Kisongo walikutana ili waweze kujadiliana matatizo mbalimbali yaliyokikabili kijiji chao.


Kabla ya saa ambayo waliahidiana kukutana, saa 9 mchana, mwenyekiti wa kijiji, katibu wake, meneja wa kijiji, katibu kata, mratibu kata wote kwa pamoja waliwahi na kukutana ili waweze kuchambua baadhi ya dondoo ambazo zitazungumziwa kwenye mkutano huo. Dondoo ziliandikwa na katibu wa kijiji kama ifuatavyo:- Kwanza ilihusu ukosefu wa kuni na mkaa, na mafuta ya taa. Pili ilihusu utekelezaji wa kazi za kila siku. Tatu ilihusu vijana kukimbilia mijini. Nne, ambayo ni ya mwisho ilihusu wanakijiji kutohudhuria kisomo.

Muda uliwadia na wanakijiji wote walikuwa wameisha wasili tayari kwa kuanza mkutano nje ya jengo la CCM. Hapo nje Mzee Ole Lengai na Mzee Shongolo waliketi na kuanza kuzungumza machache ambayo watayauliza kwenye mkutano wa kijiji. Mzee Shongolo alianza kumweleza, "Mimi lazima niulize kwa nini mzee Ngolo hakuhudhuria kwenye kazi ya kupanda shamba la kijiji, na wengine hawakufika kwenye kisomo jana?" Mara mzee Ole Lengai alidakia maneno na kusema "Hao wote walianza kunywa pombe asubuhi na niliwakuta wamelala kwenye manyasi, ni lazima tuwaseme wazi wazi." Muda si mrefu mwenyekiti akawaeleza wanakijiji wakusanyike tayari kwa kuanza mkutano. Watu wote walikusanyika na mwenyekiti na viongozi wenzake walitoka ndani na kukaa kwenye viti tayari kwa kuanza mkutano. Mwenyekiti alifungua mkutano na kusema, "Kidumu Chama cha Mapinduzi." Wanakijiji waliitikia "Kidumu" Mwenyekiti alisema tena "Zidumu fikra za mwenyekiti wa CCM," Wakaitikia, "Zidumu." Mara mwenyekiti akaanza kwa kusema "Sina muda wakupoteza sasa hivi kama mnavyotuona hapa kulia kwangu yupo Katibu Kata na wa pili Meneja wa Kijiji, kushoto kwangu kuna Katibu wa kijiji wa pili ni Mratibu Kata. Wote hawa tutashirikiana nao katika Mkutano huu. Nisingepoteza muda ningemkaribisha katibu ili aanze kutusomea dondoo zetu."

Mara katibu wa kijiji alisimama na kusalimia kichama. Kisha akasema, "Ndugu wanakijiji sina mengi ya kusema ila tu ningeanza kusoma dondoo yetu ya kwanza na tuijadili. Inahusu tatizo la ukosefu wa kuni na mkaa." Wazee wengi walinyoosha mikono lakini mwenyekiti alimchagua mzee Shongolo aweze kuchanga mawazo. Mara wazee wengine wakaanza kulalamika kuwa anamchagua yeye kwa kuwa "eti ngishu kumoku". Maana yake Sijui. Mara mzee Shongolo alisimama na kuanza kueleza kwa nini kuni siku hizi hazipatikani, akaendelea kuwa 'kuni hazipatikani kwa sababu mvua siku hizi hazinyeshi kama zamani, miti haikui inazidi kufa tu.' Wanakijiji wenzake walipinga. Mzee mmoja mwenye upara mweupe kama barafu alisimama na


kusema, hiyo sio sababu. Kuni tunakosa kwa sababu miaka ya nyuma tumefyeka sana miti na kuchoma ovyo kila mtu anavyopenda. Kama ingekuwa mvua, kwa nini sehemu zingine kuwe na miti wakati tatizo la mvua ni la Tanzania nzima? Wote wakakubaliana kuwa ndiyo sababu hasa iliyosababisha kukosekana kwa miti. Ndipo mwenyekiti akaingilia kati na kusema, "Tumeona sababu yenyewe sasa tuachieni suala hili sisi viongozi tutajadili na kutafutia utatuzi." Wote waliafiki na kushangilia kwa makofi.

Mara Katibu wa kijiji alisimama tena na kusoma dondoo ya pili iliyohusu utendaji wa kazi mbaya. Alipokaa wanakijiji bila kuchelewa waliinua mikono kutaka kusema. Mwenyekiti alimchagua ndugu Ole Lengai aweze kueleza sababu zinazofanya utendaji wa kazi usifanikiwe. Mzee Ole Lengai alisimama huku akitupia blanketi begani



na kusema "Hatufanikiwi kufanya kazi vizuri sababu ya watu wengine kutohudhuria kazini." Mzee mmoja alisimama ghafla na kupinga kwamba hiyo sio sababu. "Mimi ninavyoona ni kwamba siku hizi pombe zimezidi hasa pombe moshi na kangara. Kila nyumba inapika na watu wanalewa asubuhi sana. Watu wote walitingisha vichwa nyuma na mbele kuonyesha kwamba wamekubaliana na usemi huo. Baada ya mjadala huo wote waliafikiana kuwaachia viongozi wao wajadiliane na kutafuta utatuzi. Dondoo ya tatu iliyohusu vijana kukimbilia mjini ilisomwa. Kweli dondoo hii iliwasikitisha sana wazee wengi ambao walikuwa wamekosa msaada wa vijana wao. Katibu Kata alisema kwamba suala hili linasababishwa na wenyewe wazazi kuwaachia vijana kwenda kutafuta kazi. Kwahiyo aliomba wawaachie viongozi watafute njia ya kutatua. Wanakijiji wote hawakuwa na ubishi mwingi baada ya kuona mfano mbaya wa kijana Loitore ambaye alipigwa kwa ajiliyya wizi. Wote waliafiki na kuachia viongozi wajadiliane zaidi hadi ufumbuzi utakapopatikana.

Dondoo ya mwisho ilihusu kutohudhuria kisomo. Kweli wanakijiji waliguna kidogo sababu wale wote ambao huwa hawahudhurii kisomo kwa kudai eti wanakazi nyingi hasa za uchungaji na za kufuata kuni porini wote walikuwepo. Mzee Shongolo na mzee Ole Lengai walinyosha mikono. Mwenyekiti alimchagua mzee Ole Lengai aanze kujibu au kueleza suala hilo. Alianza kusema, "Ndugu Mwenyekiti jambo hili sio la kuzungumzia kwa urahisi, wengine wako hapa hapa hawahudhurii na mnawaona lakini hamuwasemi au kuwaonya. Mimi langu ni hili tu sina mengi." Mwenyekiti akacheka kisha akasema "sishirikiani nao, kwanza tuangalie kwa nini hawahudhurii kisomo." Ndipo mzee Lumeki akasema, "Mimi naona kutokuhudhuria kwao tuangalie nyuma matatizo yetu hasa tatizo la kuni ambalo limetukabili sana. Watu wanakwenda mbali kutafuta kuni wakirudi wamechoka hata hamu ya kuhudhuria kisomo hawana. Mimi naona kwamba suala hili litafutiwe dawa. Tumwachie mwenyekiti na viongozi wengine watafute ufumbuzi wa matatizo yote.



Sio hayo tu waliyojadili. Matatizo mengi sana yaliwakabili na yote walijaribu kutafutia ufumbuzi lakini haikuwezekana. Ndipo mwenyekiti alisema "Matatizo yote haya nitajaribu kuwasiliana na wataalam wanaohusiana nayo ili tuweze kushirikiana na kutafuta ufumbuzi." Ndipo mwenyekiti aliahirisha mkutano hadi utakapofanyika tena siku nyingine.

## SURA YA TATU

## WANAKIJIJI WAALIKA WATAALAM

Hauchi hauchi unakucha. Siku ambayo imepangwa wanakijiji kukutana na wataalam iliwadia. Mabalozi wote walipitia nyumba zao kumi kumi, na kutoa taarifa za mkutano siku moja kabla. Kila mwanakijiji alilala akiwa na taarifa ya mkutano.

Ilipofika saa nane mchana, vigoma vilisikika kwa upande wa kijiji. Vigoma vilipotulia, sauti nyororo ya kijana aliyekuwa akipiga la mgambo ilitawala hewa yote ya kijiji.

Naam, kila sikio linasikia wazi maneno haya. "Haya leo! Haya leo! ya kesho ni ya mzembe na mwongo. La mgambo likilia lina jambo. Asiye na mtoto abebe jiwe. Asiye na jicho aweke la kondoo; asiye na mguu aweke tendegu. Ndugu wanakijiji ahadi ni deni. Kama tulivyokubaliana na kuahidi kualika wataalam kutusaidia kujadili mambo fulani siku yenyewe ndio leo. Nao wameshafika. Kama walivyosema wahenga, 'Mvunja ahadi ni kafiri', kweli viongozi na wataalam hawa hawakupenda kuvunja ahadi zao. Mkutano ni saa tisa jioni. Wanakijiji wake kwa waume, mnashauriwa kuwa uwanjani, chini ya mti mkuu, kama kawaida yetu; saa tisa bila kukosa. Tisa bila kukosa narudia."

Hata kabla ya saa tisa wanakijiji walianza kumiminika kwa wingi kuelekea chini ya mti mkuu. Kila mmoja alichukua nafasi yake kama alivyopenda. Muda si muda, mti mkuu ukawa umesimama katikati ya umati mkubwa wa wanakijiji, waliojawa na hamu ya kuwaona na kuwasikia wataalam na viongozi. Matawi yake yalikuwa kama mwamvuli mkubwa ukiwakinga wasipatwe na jua ambalo wakati huu lilikuwa kali sana. Vijana walipanga meza na viti karibu na shina la mti.

Wakati walipokuwa wanasubiri viongozi wao wa kijiji pamoja na wageni, alijitokeza msichana mmoja kwa jina Ngaisungui. Huyu Ngaisungui alisifika sana kijijini kwa kuwa na heshima, upole, usikivu, ukakamavu pamoja

na moyo wa kupenda kazi. Alishahudhuria mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na wenzake. Kinyume cha wenzake waliokimbilia mijini baada ya kumaliza mafunzo yao, yeye alirudi kijijini akajiunga na wanakijiji katika shughuli mbalimbali. Binti huyu aliwaomba wanakijiji kwa utulivu, akisema. "Baba zangu, mama zangu, kaka zangu, dada zangu na vijana wenzangu. Mnaonaje tukiimba wimbo mmoja mfupi wa kutuchangamsha kabla viongozi na wageni hawajafika?" Sauti za kunguruma zilizochanganyika na sauti nyororo ziliitikia ushauri huo.

Akaanza wimbo, "Chama chasema, kisomo! kisomo!" wanakijiji kwa pamoja wakaitikia "eeeee kisomo, kisomo, kisomo kwa wote." "Nyerere asema kisomo! kisomo', "eeee kisomo kisomo kisomo kwa wote."

"Na Jumbe asema kisomo! kisomo!" "eeeee kisomo kisomo kisomo kwa wote" x 3. Wakaendelea hivi wakipiga makofi. Mara katibu wa kijiji akatokea akiwa na wageni sita wakifuatiwa na mwenyekiti. Hapo tena wimbo uliachwa makofi yakatawala uwanja. Vijana waliweka mbwembwe katika upigaji wa makofi hadi wazee wengine wakaanza kucheka.

Baada ya kukaa kwenye viti, Mwenyekiti wa kijiji akafungua mkutano. Kwanza aliwapongeza wanakijiji kwa kuwahi. Pili, aliwashukuru viongozi na wataalam walioalikwa kwa kuitikia wito. Alipomaliza aliwatambulisha wageni wote. Alianza na Bwana shamba, Afisa wa Ujamaa na Ushirika, Bwana miti, Katibu wa Chama cha Uzazi na Malezi Bora (UMATI), Afisa Mifugo na kuishia na Katibu wa vijana. Akamwomba bwana shamba asalimiane na wanakijiji kwa niaba ya wageni wote kabla ya shughuli kuanza.

Bwana Shamba alisimama na kuinua mkono wake wa kulia uliokunja ngumi na kusema, "Kidumu Chama cha Mapinduzi,"

Wanakijiji wakaitikia, "Kidumu."

"Kisongo safii?" akauliza bwana shamba.

"Safiii!

"Kisomo jee?"

Zilisikika sauti zilizochanganyika na miguno na manung'uniko zikitoka kwa wananchi.

"Asanteni," alisema Bwana Shamba na kukaa.

Hapo Katibu wa kijiji alisimama na kuanza kuzungumza na wanakijiji na wageni akisema, "Ndugu wanakijiji, mtakumbuka katika mkutano wetu uliopita tulizungumza mambo yafuatayo:

1. Shida au tatizo la upatikanaji wa kuni.
2. Utendaji wa shughuli zetu za kila siku hapa kijijini.
3. Tatizo la kutoshiriki kisomo baadhi ya wanakijiji.
4. Tatizo la vijana wetu kukimbilia mijini, hasa baada ya kumaliza masomo yao ya darasa la saba.

"Hayo tuliyajadili vya kutosha tukaelewa makosa yalipoanzia ingawaje hatujaamua utatuzi wake. Tulikubaliana kuwa tutoe ufumbuzi wa pamoja, baada ya kumalizia mengine matatu yaliyobaki. Nayo ni:

1. Uchaguzi wa mazao ya chakula na biashara na kufuata majira ya kilimo.
2. Tatizo la kutokuzaa kwa majira.
3. Upatikanaji wa bidhaa muhimu na mengineyo kama tutakuwa na nafasi kwa ruhusa ya mwenyekiti."

Hapo mwenyekiti akasema bila kupoteza muda, "Tunaomba Bwana Shamba utupatie mawazo juu ya dondoo la kwanza: UCHAGUZI WA MAZAO YA CHAKULA NA BIASHARA NA KUFUATA MAJIRA YA KILIMO."

Bwana Shamba akasimama na kusema, "Ndugu Mwenyekiti, ndugu Katibu, Wanakijiji wapendwa na wageni wenzangu. Suala hili tukitaka kujua namna ya kulikabili sharti tuelewe linasababishwa na nini au tujue chanzo chake. Inakuwa vizuri zaidi kama tutajadili kwa pamoja."

Mzee Lobikoki ndiye aliyekuwa wa kwanza kunyoosha mkono na baada ya kuruhusiwa akasema, "Mwenyekiti, wageni na wanakijiji wenzangu. Tatizo hili linakuwa kubwa zaidi kwa kuwa hatupati ndizi, maharage na mahindi kwa wingi. Chakula chetu tulichozoea ni loshoro, ambacho hupikwa kwa kuchanganya mazao haya matatu, ndizi, maharage, mahindi pamoja na maziwa mgando. Na chakula cha kitalolo, hiki hupikwa kwa kuchanganya maharage, ndizi, mahindi, maziwa mabichi pamoja na mboga za majani. Vingine havitufai. Tumezoea kulima wakati wote

wa vuli na masika. Sasa hii in kasoro gani?" Wanakijiji wanapiga makofi.

Mtaalam wa kilimo akajivuta na kumshukuru mzee kwa mchango mzuri wa mawazo. Kisha akaeleza, "Mazao mnayolima hapa kijijini ni safi kabisa, kasoro ni kidogo tu, nayo ni kwamba:

"Mnalima wakati wa masika na vuli tu. Je wakati mwingine hatungeweza kulima mazao mengine kama mihongo, mtama, ulezi ambavyo wakati wa ukame bado vingevumilia na kusitawi. Tena tungeongeza mazao mengine kama viazi mviringo (mbatata), viazi vitamu badala ya kulima migomba, maharage na mahindi tu. Kwa muda mrefu kijiji kimetegemea kitu kimoja tu au viwili. Tukumbuke kutaka si kupata. Mwenye njaa hana miiko. Miiko tunayojiwekea inatufunga mahali pamoja."

Wanakijiji wakasikika wakisema kwa sauti za juu, "Kweli kabisa! Watu wa shida? Tena bado tunachagua hata vyakula!"

Hapo tena Mwenyekiti aliwaomba watulie. Katibu akasoma agenda ya pili ambayo ilihusu TATIZO LA KUTOZAA KWA MAJIRA kijijini. Baada ya kumkaribisha katibu wa chama cha Uzazi na Malezi Bora (UMATI). Mtaalam akasimama na kusema, "Tatizo hili ni kwamba wanakijiji wengi wameacha mila zetu za zamani na kuzipuuza. Kwa mfano: (1) Zamani mwanamke akijifungua huenda kupumzika kwa wazazi wake kwa muda. Ilikuwa aibu na marufuku mama kupata mimba kabla mtoto wa kwanza kutembea. Wastani huu ni kama miaka miwili. (2) Wamepuuza au kudharau dawa za asili zilizotumika kuzuia kupata mimba, ambazo zilikuwa za kunywa na hata za kuvaa. (3) Kutohudhuria kliniki na kupata mawazo na mafunzo ya mpangilio wa uzazi toka kwa wataalam. Ya mwisho ingawa ni ya kuchekesha ni kutokuwa na shughuli nyingi za kazi kila saa bwana na mkewe. Pamoja na hayo utatuzi tunaweza kuufikia, lakini hebu tutupie macho dondoo ya mwisho."

Katibu alisimama na kusema, "Dondoo yetu yahusu upatikanaji wa bidhaa muhimu kwani wanakijiji wengi wana-

lalamika kwamba bidhaa hazifiki kwenye maduka yao ya Ushirika, au pengine hufika kwa uchache sana kiasi ambacho wanashindwa kuzigawanya."

Bwana Ujamaa na Ushirika aliwatoa wananchi wasiwasi kwa kuwaeleza kwamba: (1) Bidhaa zinakuwa chache kwa kuwa watu wengi wanazitumia, mfano sabuni, - watu wengi zamani hawakutumia sabuni za kufua, na kuoga. Siku hizi kila mtu amejua manufaa ya sabuni. (2) Sukari - zamani wazee wetu walitumia miwa na asali mwitu. Siku hizi kila mtu anatumia sukari. (3) Mafuta ya kupikia kwa mfano, zamani watu wengi hawakutumia mafuta ya madukani, leo kila mtu anahitaji. (4) Kanga - akinamama wa zamani hawakuvaa sana kanga, leo kila mama anazihitaji. (5) Mavazi kwa ujumla watu wengi zamani hawakuhitaji leo kila mtu huhitaji. Hivyo kama watu wote itabidi wapate vitu hivi, na mali ghafi ya kutengenezea vitu hivi hatuna ya kutosha; hamuoni kuwa chanzo kinakuwa wazi zaidi? (6) Pia kuna ufichaji wa bidhaa kwa baadhi ya watu ambao ni wenyewe wanakijiji. (7) Kukubali kununua bidhaa kwa bei ya kuruka, kunaweza pia kuwapa moyo wagongaji. (8) Kutowafichua wagongaji ni tatizo jingine. (9) Kutokujua namna au mpango mzuri wa kugawanya bidhaa hizi ili kila mtu apate, hata kama ikibidi kwa zamu. Sio mtu mmoja apate kila mara."

Hapo vifijo na makofi vikapigwa na wengine kusema, "Tunauana wenyewe, tunagongana wenyewe, tunadhulumiana wenyewe. Kweli lazima tukubali mabadiliko."

Kwa kuwa muda ulikuwa umekwisha mwenyekiti wa kijiji aliwaomba wanakijiji wasiwe na maswali mengi ili waweze kujadili utatuzi wa maswala yote kwa ujumla. "Tutaanzia na yale ya mwanzo hadi ya mwisho kwa kukumbushana tu tutaanza na tatizo la upatikanaji wa moto au kuni kwa wastani."

## SURA YA NNE

## UFUMBUZI WA MATATIZO

Matatizo ya wanakijiji yamefahamika. Pia vyanzo vya matatizo vimejulikana kijijini. Mzee Kirobo alipewa nafasi ya kuzungumza. Katika mazungumzo yake, alizingatia tatizo la kuni na mkaa. Alianza kwa kusema, "Wanakijiji wenzangu niliwahi kutembelea kijiji cha Olgilai miaka mitano iliyopita. Walikuwa na tatizo kama hili. Hapakuwa na miti, vumbi lilikuwa jingi, na kuni ilikuwa tatizo kabisa. Juzi, nilikwenda huko na nilishangaa kuona jinsi kilivyokuwa na misitu." Baadhi ya wanakijiji waliinua mikono wakisema, "Ni kweli." Mzee Kirobo aliendelea na kuesema "Wenzetu walishauriwa na mtaalam wa miti kuwa wapande miti. Hivyo walizingatia ushauri huo."

Mzee Kirobo alimalizia kwa kusema, "Sasa hivi hawana shida ya kuni wala mkaa. Vumbi nalo hakuna tena. Miti ya kujengea ipo tele na maji ni mengi sana." Mama Naisoi alidakia na kusema, "Tena wana bustani ya miti. Kwa nini na sisi tusianzishe bustani yetu? Lazima tumwone mtaalam wa miti." Wanakijiji wote waliunga mkono wakisema, "Sawa" na kushangilia kwa kupiga makofi na vigelegele. Ndipo mwenyekiti akasisitiza na kutilia mkazo juu ya uanzishaji wa bustani ya miti katika kijiji chao. Pia wanakijiji walikubaliana kuwa upandaji wa miti upewe umuhimu wake. Ukataji miti uwe na utaratibu maalumu. Uchomaji moto misitu michache iliyobaki ukomeshwe. Mwenyekiti alimalizia kwa kusema, "Hatua kali itachukuliwa kwa yeyote atakayekiuka maazimio haya."

Balozi Lesion alipata nafasi ya kutoa hoja yake. Alianza kwa kusema, "Shughuli zetu hapa kijijini zimelala. Ndugu Mwenyekiti, watu siku hizi ni wategaji. Wanashinda kwenye pombe na kuzurura ovyo. Kazi hazifanyiki. Shamba letu la Ujamaa limekuwa msitu. Ni aibu."

"Tboa," wanakijiji waliitikia kwa sauti moja.

"Balozi aliendelea na kusema, "Tuondoe tatizo hili."

Katibu wa kijiji alisimama kwa idhini ya Mwenyekiti. Alianza kwa kusema, "Wanakijiji wenzangu, tatizo hili

lipo na leo litafutiwe dawa."

"Sawa katibu", wanakijiji waliitikia.

"Mimi nashauri tuzingatie kikamilifu utaratibu na mpango wa kazi kama tulivyopanga mwaka juzi. Kwa kuwakumbusha, Jumatatu, Jumatano na Ijumaa ni siku za shughuli zenu wenyewe. Pia vilabu vyote hapa kijijini, vifungwe hadi saa kumi jioni. Pamoja na hayo kila mwanakijiji afanye kazi kwa bidii siku zote."

Baada ya kukumbushwa hayo yote wanakijiji walikubaliana kuyazingatia. Mara Katibu alipokaa, alisimama Mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama kijijini. "Ndugu wanakijiji, mipango hiyo inaeleweka. Tunaelewa usemi wa chama wa kila mtu afanye kazi. Huenda tumejisahau. Kuanzia sasa kamati yangu itazingatia sana sheria inayotawala utendaji wa shughuli zetu hapa kijijini." Wanakijiji walijadiliana suala hili kwa kirefu na wakakubaliana kufuata taratibu za utendaji wa shughuli za kila siku kama awali.

Katibu wa kikao, alieleza tatizo la vijana kukimbilia mijini. Kwa idhini ya mwenyekiti alisimama ndugu Mkandawile na kusema, "Tatizo hili ni letu wenyewe. Kijiji chetu kina ardhi ya kutosha na yenye rutuba. Pia tunaweza kuomba mkopo na kuanzisha miradi ya kiuchumi.

"Miradi hii ni kama vile ufugaji, ushonaji, ufinyanzi, uashi na kadhalika. Kwa njia hii vijana wetu watakuwa na shughuli za kufanya hapa kijijini. Je, wanakijiji wenzangu, hayo hayawezekani?"

"Yawezekana kabisa. Mipango iandaliwe," wanakijiji waliunga mkono na kujibu kwa furaha.

Ndipo mama Nangoko alipata nafasi ya kuzungumza. Katika hoja zake aliongezea kuwa kijiji pia kianzishe soko. Soko hilo litakuwa la biashara za vitu mbalimbali vipatikanavyo hapo kijijini. Hivyo vijana wanaweza kujiunga kwa vikundi na kuendesha shughuli mbalimbali za kibiashara. Pamoja na hayo mama Nangoko alishauri Jumuiya ya vijana iimarishwe hapo kijijini. Katika kufanya hivyo mafunzo mbalimbali yatatolewa kwa vijana kupitia jumuiya yao. Michezo na starehe viwepo kijijini ili vijana wao-

ndokane na tabia ya kutorokea mijini kufuata vitu hivyo. Hoja za mama Nangoko ziliungwa mkono na kikao kwa jumla. Katika mjadala wa kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo, mzee Lekareu naye alipata zamu ya kuzungumza. Kwa mshangao aliuliza, "Je, vijana hawa wanapotorokea mijini, wanatokea wapi?"

Baadhi ya wanakijiji walijibu, "Majumbani kwetu."

Mzee Lekareu aliendelea, "Basi huenda sisi ndiyo tunaoruhusu vijana kutorokea mijini. Ni lazima kuwashirikisha katika shughuli zetu za kila siku pale majumbani mwetu. Washiriki katika kulima, kuchunga, kuchota maji na kadhalika. Pia kila mzazi awe mshauri wa mwanawe na vijana wengine juu ya madhara na taabu za kuzurura mijini bila kazi. Kwa njia hii tutatoa mchango wetu katika malezi ya vijana wetu hawa."

Baada ya hoja za mzee Lekareu, Mwenyekiti wa kikao alielezea kikao jinsi ofisi yake inavyojitahidi kukabili tatizo hilo. Aliwaarifu wanakijiji kuwa tayari orodha ya vijana wote toka kila shina ipo. Jumuiya ya vijana ipo. Mipango ya kuanzisha baadhi ya miradi imeandaliwa.

Kwa idhini ya mwenyekiti, kijana Loitore alipata nafasi ya kuchanga mawazo yake. "Mimi nikiwa kijana, nafurahi kuona kuwa mnatambua tatizo hili. Kwa kuanzia naomba kikao hiki leo kitupatie ardhi. Bila shaka tutajiunga na kuanza kutayarisha kwa msimu ujao."

"Sawa babaa!!" Vijana wenzake waliitikia kwa shangwe.

"Tena tutalima kwa utaalam kwani sisi tumeelimika. Na uchumi tutainua" Loitore aliongeza.

Kutokana na majadiliano hayo marefu, wanakijiji walikubaliana kuwa ombi la vijana litekelezwe mara moja. Pia waliiarifu kamati ya mipango na fedha izingatie na kuharakisha uanzishaji wa miradi ya kiuchumi hapo kijijini. "Chama na Serikali vihakikishe kuwa hakuna vijana wanaozurura mijini," Mwenyekiti alimalizia.

Mwalimu wa darasa la Balozi Olotu alinyoosha kidole. Mwenyekiti alimpa nafasi ya kuzungumza. "Hebu toa hoja," Mwenyekiti alimruhusu.

"Hapa kijijini tuna madarasa ya kisomo. Kuna baadhi ya wanakijiji hawashiriki katika kisomo. Ndugu Mwenyekiti tufanyeje?"

Kutokana na swali hilo wanakijiji walitoa hoja na mashauri mbalimbali kuhusu umuhimu wa kisomo. "Anayekataa kisomo ni mjinga sana," alisema mama Naimutie. "Hawezi kujua mema na mabaya. Kwa jumla hatakuwa na maendeleo yoyote," Alimalizia mama Naimutie. Mzee Ndooki aliongezea kwa kusema, "Mimi nilianza kisomo 1971. Mpaka leo nasoma. Nimejua kusoma na kuandika. Nimejua kulima bustani. Nimetambua faida ya kula chakula bora."

Mwenyekiti alimruhusu mzee Lembinyo kuzungumza. Ndugu Lembinyo aliuliza, "Nikijua kusoma na kuandika nitapewa kazi gani? Je, nitakuwa mwenyekiti wa kijiji au daktari?"

Wanakijiji waliangua kicheko kwa maswali ya Mzee Lembinyo. Mwenyekiti alimfahamu mzee huyo kuwa yeye ni mlevi wa gongo. Hivyo alimweleza kwa kifupi manufaa ya kisomo. Kikao kiliendelea kujadili kwa kirefu ufumbuzi wa tatizo hili. Mwishoni waliamua kuwa kisomo ni jambo zuri. Huwaondolea watu ujinga. Kisomo huleta maendeleo. Pia huleta uchumi. Wanakijiji walikubaliana kuwa kila mwanakisomo ashiriki katika kisomo. Wale watakaolegalega kama Mzee Lembinyo wataadhibiwa kwa kufuata sheria za kijiji.

Wanakijiji wamefanikiwa kufumbua baadhi ya matatizo. Mwenyekiti wa kijiji aliwakaribisha wataalamu kutoa ushauri wao. "Karibu Ndugu Afisa Ujamaa na Ushirika," Mwenyekiti alitamka.

Afisa Ujamaa na Ushirika alisimama na kuanza kutoa hoja. "Ndugu wanakijiji mnaelewa kuwa tuna tatizo la kupata vitu muhimu. Hili ni tatizo la kitaifa. Hata hivyo baadhi ya matatizo, tunaongezea sisi wenyewe. Ili kupunguza malalamiko, vile vitu vichache vinavyopatikana vifike kwenye duka la kijiji. Kamati ya duka ihakikishe kuwa vitu vinagawanywa kwa haki bila upendeleo." Wanakijiji walikazia kwa pamoja wakisema,

"Vigawanywe kwa zamu kwa kila balozi." Afisa Ujamaa na Ushirika aliendelea, "Wahudumu wa duka waepukane na tabia ya ufichaji bidhaa. Bidhaa zote adimu zifikapo dukani zigawanywe bila kufichwa. Kamati ya duka iwe macho sana. Ulanguzi na ugongaji upigwe vita hapa kijijini. Wanakijiji wasiwe na tamaa ya kununua vitu kwa wingi. Endapo watafanya hivyo, itasababisha wengine kukosa. Kwa njia hii tatizo hilo linaweza kuwa na unafuu." Wanakijiji walipiga makofi na kuahidi kuwa watazingatia mashauri hayo.

Baada ya hayo, mtaalamu wa kilimo alikaribishwa. Ndipo aliposimama na kuanza kusema, "Tutilie mkazo kilimo bora. Tutayarishe mashamba kwa kufuata majira. Katika kufanya hivyo mtakuwa tayari kupanda mara mvua zianzapo kunyesha. Mashamba yaendelee kutunzwa hadi wakati wa mavuno. Tuvune mazao mara yanapokomaa. Tuhakikishe kuwa tuna hifadhi vema mazao ya kutosha kwa chakula. Endapo kutakuwa na ziada, tuuze kwenye shirika la Umma. Kwa nyakati za ukame tulime mazao yanayostahimili ukame, kama vile mtama, viazi, mihogo na serena."

Mtaalamu wa kilimo pia aliwaeleza wanakijiji juu ya matumizi ya chakula. "Wakati huu mgumu kiuchumi, tusichague chakula. Kuna watu waliozoea kula wali, kwa sasa hivi kuna upungufu wa mchele. Hivyo wale kile kinachopatikana kama vile ugali, mihogo au ndizi. Tujenge tabia ya kula kile tulichonacho. Tuache kudai kitu ambacho hakipo." Mwisho alikazia mtaalam huyo kwa kuwataka wanakijiji wazidishe juhudi na maarifa katika kufanya kazi kwa pamoja. Aliwaachia methali isemayo "Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu."

Kutokana na hoja za mtaalamu huyo, wanakijiji waliafiki kuimarisha kilimo. Pia waliomba pembejeo zisambazwe mapema kabla msimu wa kilimo kuanza. Baada ya hapo Mwenyekiti alimshukuru mtaalamu kwa ushauri wake. Aliwaomba wanakijiji wazingatie hayo na kuomba ushauri kila wanapokuwa na matatizo.

Kutokana na maelezo ya mwenyekiti Mzee Ngorocho alitaka kufahamu, "Je, tunawezaje kupata utaalamu wa kutumia maksai katika shughuli zote za kilimo? Hii nimeuliza kwa sababu, huwa tunatumia maksai kwa kulima na kupanda. Je, hatuwezi kutumia maksai kwa kupalilia?"

Mtaalamu wa kilimo alisimama na kushukuru kwa swali hilo. "Tunaweza kabisa kutumia maksai," alijibu mtaalamu.



"Kinachotakiwa ni kupata jembe maalum la kupalilia. Jembe hili la kupalilia litakokotwa na maksai. Ili maksai wasile mazao itabidi kufunga midomo yao. Ikiwa mtahitaji kupata ujuzi huo, niko tayari siku yoyote kuwaelimisha."

Wanakijiji walifurahishwa sana na usemi wa mtaalamu na kusema, "Tutashukuru sana ukija kutuelimisha kuhusu suala hili."

Mwenyekiti aliwaomba wanakijiji wavumilie kidogo ili wasikie hoja za Katibu wa Chama cha Uzazi wa Majira na Malezi Bora. Bila kupoteza wakati, mwenyekiti alimkaribisha katibu huyo aendelee kuwashauri wanakijiji. Katibu alianza kwa kuelezea maana ya uzazi wa majira. Alisema, "Uzazi wa Majira si kuacha kuzaa. Uzazi wa majira ni kuzaa watoto kwa wakati unaofaa. Kuna faida nyingi za kuzaa kwa muda maalum. Mojawapo ni kuwa mama atakuwa na afya. Hivyo atakuwa na nguvu za kufanya kazi. Pia mtoto atatunzwa vizuri. Baba naye atakuwa na nafasi nzuri ya kushughulikia familia. Ataweza kulisha, kuvisha, kuelimisha na kuitunza familia yake kwa ujumla."

Katibu aliendelea, "Ili kufanikisha mpango huu, mama na baba washirikiane kujadili."

Baada ya Katibu kumaliza kuzungumza, alisimama ndugu Boki. Ndugu Boki ni mmojawapo wa wanakijiji. Hupenda sana kuzingatia mashauri kuhusu uzazi wa majira. Ndipo aliwashauri wanakijiji wenzake kwa kusema, "Ushauri wa mtaalamu ni muhimu. Mimi napenda kuongezea kidogo." Aliinama kidogo na kusema, "Mafunzo kwa wazazi ni jambo muhimu. Nasema wazazi! Baba na mama. Ni muhimu kuhudhuria mafunzo ya kliniki katika kituo cha afya. Mafunzo haya tunaweza kuyapata katika kituo cha afya kilichoko hapa hapa kijijini. Mke wangu na baadhi ya akina mama wengine hapa wamefaidika sana na mafunzo haya. Hata mimi nimefaidika kwani nimejikwamua kutokana na madhara ya kuzaa kila mwaka. Watoto nilionao sasa hivi naweza kuwalea vizuri. Jamani wanakijiji tuzingatie ushauri wa Katibu wa Chama cha Uzazi wa Majira na Malezi Bora." Mwisho mwenyekiti wa kijiji alisimama. Ndipo alianza kwa kuwashukuru wataalamu na wanakijiji. Alisema kuwa kikao hicho kimefanikiwa sana. Aliendelea kwa kusema kuwa katika mjadala wao, wanakijiji wazingatie utekelezaji wa maazimio yao. Alimalizia kwa kunyoosha mkono uliokunja ngumi juu na kusema,

"Kidumu Chama cha Mapinduzi." Wanakijiji waliitika "Kidumu." Mwenyekiti alitamka "Kikao kimefungwa." Ndipo wajumbe walianza kutawanyika wakisemezana na kufurahi.

## WALIOSHIRIKI KATIKA WARSHA YA UANDISHI WA KITABU

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Richard R. Ringo | - | Mratibu Kata Mbulu |
| 2. | Lee Williams | - | Mwalimu Oldeani Mbulu |
| 3. | Mary Kaswende | - | Mwalimu Ngarenaro Shule ya Msingi Arusha |
| 4. | Joseph Mollel | - | Mratibu Kata Arusha |
| 5. | Mariam H. Kirumo | - | Mwalimu Uhuru Shule ya Msingi |
| 6. | Amina Juma | - | Mwalimu Themi Shule ya Msingi |
| 7. | Japhet Makala | - | Mwalimu Enguiki Shule ya Msingi |
| 8. | A. Chale | - | Afisa Misitu Arusha. |

## VIONGOZI WA WARSHA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Lawrence L. Kagaruki | - | Mratibu wa Warsha<br>Mkufunzi Mkuu wa<br>Idara ya Elimu kwa<br>Umma-TEWW, D'Salaam. |
| 2. | N.E. Mcharo | - | Mkufunzi<br>Mkuu wa Idara ya Mafunzo<br>TEWW - Dar es Salaam |
| 3. | Susan Kayetta | - | Mkufunzi<br>Idara ya Elimu kwa Umma<br>TEWW - Dar es Salaam |
| 4. | Mohamed Gulleth | - | Mkufunzi<br>Mkuu wa Kituo<br>TEWW - Arusha. |